

KAULI ZA MAWAZIRI

Viwango vya Chakula kwa Wafungwa Magerezani

SPIKA: Jana wakati wa kipindi cha maswali, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alieleza kuhusu mambo ya Magereza na kukatokea ombi la Mwingozo wa Spika hapa kuhusu suala alilolisema kutoka kwa Mheshimiwa Vincent Nyerere. Tulimwagiza Waziri aje atoe kauli kuhusu suala hili. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa Kauli ya Serikali kuhusu mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini.

Jana tarehe 1 Novemba, 2012 katika maswali ya nyongeza, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, aliuliza; nanukuu Hansard ya tarehe 1 Novemba, 2012: "Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali itamke rasmi kwamba, kilichosemwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba wafungwa na mahabusu wanapaswa kula milo mitatu ndiyo amri ya Serikali. Naomba Serikali itamke hilo."

Mheshimiwa Spika, kutokana na swali hilo nilijibu kama ifuatavyo, nanukuu: "Mheshimiwa Spika, taratibu za namna ya kula na kuishi katika magereza yetu, zinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uendeshaji wa Magereza na hazitamkwi Bungeni. Mwisho wa kunukuu."

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba kuondoa maneno hazitamkwi Bungeni kwa kuwa hakuna mamlaka inayoweza kulizuia Bunge lako kuzungumza mambo ya magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuondoa maneno hazitamkwi Bungeni, sasa naomba kutoa taarifa kwamba, viwango vya chakula kwa wafungwa magerezani, vinaweka kwa mujibu wa *Prisons Regulation* za mwaka 1968, kifungu cha 23(1), zilizotungwa kwa mujibu wa Sheria ya Magereza (*Prison Act*) ya mwaka 1967. Viwango hivi vimewekwa kwa mujibu wa Sheria. Wafungwa wanakula milo miwili; kwa kawaida wanastafutahi na kifungua kinywa gramu 450, ambayo ni sawa na gramu 150 za unga wa uji na gramu 300 za vitafunwa. Mchana wanapata gramu 500 ambazo ni milo miwili ambayo ni gramu 250 mchana na gramu 250 usiku. Ratiba ya chakula na muda wa kula huzingatia idadi ya wafungwa walioko gereza, idadi ya vifaa, ratiba ya kazi za wafungwa na mazingira ya usimamizi na usalama wa wafungwa na mahabusu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla chakula cha wafungwa kinatoa virutubisho vinavyohitajika. Mpangilio wa ratiba ya kula hauathiri kiwango cha chakula kinachopangwa kisheria na kinachohitajika kwa afya njema ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza linaendeshwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu. Siyo vizuri mkituambia toa amri, toa tamko na sisi tunatoa, siku moja mtatuhaji kwa nini mmevunja sheria halafu tukijibu mlituagiza mtatushangaa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao katika kuboresha hali za wafungwa magerezani ili dhamira ya kuwarekebisha ifikiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaza jana kuwa, baada ya kuahirisha kikao hiki tutakuwa na semina kuhusu Mifuko ya Hifadhi yote, tutakwenda kupata elimu tuweze kuwa na upeo wa kuelewa mambo na hasa ukizingatia juzi Mheshimiwa Dkt. Mbassa aliuliza swali, nadhani pale ni wakati wake sasa kuweza kupata urefu wa suala hilo. Kwa hiyo, nasitisha Kikao cha Bunge mpaka kesho, kumbe kesho aah, mambo yameenda haraka tena wiki hii! Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.10 Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 5 Novemba, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*